

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

17 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 17 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

362. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari Simbay, Sumaye na Mary Nagu zilizopo Hanang’ kuwa za Kidato cha Tano na Sita.

363. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita kwa kuzingatia umoja na kulinda utaiifa wetu.

364. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mchombe hadi Ijia - Mlimba yenye Km 2.7 kwa kiwango cha lami.

365. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Kituo cha Afya Kata ya Kirua - Vunjo Kusini kitajengwa.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

366. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wanaojitolea wanapewa kipaumbele cha kupata ajira pindi nafasi za ajira zinapotolewa.

WIZARA YA MAJI:

367. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji uliopo katika Kata za Msongozi na Mangae - Mvomero.

368. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Visima viwili vya maji vilivyoanza kujengwa Mwaka 2021 Kikombo - Mpwapwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

369. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi - Mwibara.

370. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu Wahamiaji Haramu waliomaliza vifungo vyao na bado wapo Magerezani.

WIZARA YA UJENZI:

371. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaweka taa za kuongoza magari na taa za Barabarani katika Mji wa Tarime kwani Mji huo unapita magari mengi ya abiria na biashara.

WIZARA YA KILIMO:

372. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuweka *Block Farm* ya korosho pamoja na kupeleka Trekta Kalangasi – Igalula.

WAZIRI WA FEDHA:

373. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itawaondolea usumbufu wa kikodi Wananchi wanaobeba vitu vya matumizi binafsi wanaposafiri kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

WIZARA YA AFYA:

374. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini eneo maalum litatengwa Hospitali za Muhimbili na MOI kwa Watu wasio na ndugu Dar es Salam wanaopeleka Wagonjwa kwa matibabu.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

375. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kushughulikia mgogoro wa ardhi kati ya Hifadhi na Wananchi wa Mtaa wa Mongoroma.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
17 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**